



## SHULE ZA UMMA ZA PROVIDENCE **MAWASILIANO YA DHARURA: KILE AMBACHO FAMILIA WANaweza KUTARAJIA**

**Hali ya dharura katika shuleni mwa mtoto wako ni hali ya kuleta msongo kwa mzazi au mlezi yeyote. Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence inajitolea kukupa taarifa wakati na baada ya hali za dharura.**

- Wakati wa hali ya dharura kama vile kufungwa kwa shule au kisa cha polisi katika eneo karibu na shule, familia zitaarifiwa ndani ya dakika 15 (inapowezekana) kupitia ujumbe wa maandishi wa moja kwa moja.
- Kumbuka kwamba maelezo kamili huenda hayatapatikana mapema, kwa sababu viongozi wa majengo wanashughulika ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi na wafanyakazi.
- Wakati wa hali ya dharura inayochukua muda wa zaidi ya nusu saa, familia zitapokea ujumbe mfupi wa maandishi kila baada ya dakika 30 huku taarifa za hivi punde zikipatikana.
- Ujumbe wa mwisho wa hivi karibuni utatumwa wakati hali ya dharura imetatuliwa.
- Shule itatoa barua ya ufuatiliaji kwa familia zote ndani ya saa 24 za dharura yenye muktadha wa ziada wa tukio hilo na maelezo ya majibu ya shule.
- *Mazoezi ya dharura: Familia zitapokea ujumbe wa arifa mwishoni mwa siku yoyote ya shule wakati zoezi la dharura kama la moto au kuhamishwa linatekelezwa. Shule zinatakiwa kufanya mazoezi 15 ya dharura kila mwaka.*

### **Kile ambacho familia zinapaswa kufanya na hazipaswi kufanya wakati wa dharura:**

Kwa usalama wa kila mtu anayehusika na ili kudumisha utaratibu, tunaomba kwa heshima familia zitii mapendekezo yafuatayo wakati wa dharura:

- Hakikisha kwamba taarifa ya mawasiliano kwenye faili katika shule ya mtoto wako ni ya sasa kila wakati ili uweze kufikiwa bila kuchelewa kukitokea hali ya dharura.
- Usije kwenye kampasi ya shule. Umati unaweza kukengeusha wafanyakazi na wahudumu wa kwanza kutokana na majukumu yanayohitajika ili kuweka kila mtu salama.
- Usipige simu kwa ofisi za shule. Wafanyakazi huenda wakawa na shughuli nyingi kuhusiana na hali ya dharura.
- Usiwasiliane na wanafunzi au wafanyakazi kupitia simu ya mkononi au mitandao ya kijamii. Lazima wawe tayari kupokea maagizo kutoka kwa mfanyakazi au mamlaka kwenye eneo la tukio.
- Ifanye shule iwe chanzo chako cha habari unachokiamini. Epuka machapisho ya mitandao ya kijamii kuhusu hali ya dharura. Taarifa katika mitandao ya kijamii zinaweza kuwa zisizotegemewa sana na husambaa haraka.

### **Endelea Kupata Taarifa**

PPSD hutuma mawasiliano ya dharura kupitia programu ya ujumbe wa maandishi ya Kinvo. Wazazi huandikishwa kiotomatiki katika Kinvo mtoto wao anaposajiliwa shuleni. Iwapo unahitaji kujisajili ili kupokea ujumbe wa Kinvo, wasiliana na shule ya mtoto wako au wasiliana na timu yetu ya huduma kwa wateja kwa kutumia programu ya Let's Talk! kwa ajili ya iPhone au Android.



Scan here to view a translation in Arabic, Swahili, Khmer, Haitian Creole, & Portuguese. Escanee aqui para ver una traducción en árabe, swahili, jemer, crioulo haitiano y portugués. Changanua hapa ili kuona tafsiri kwa Kiarabu, Kiswahili, Kikhermer, Kikrioli cha Haiti na Kireno. *Klike isit la pou w wé yon tradiksyon an Arab, Swahili, Khmer Kreyòl Ayisyen ak Pòtigè.* Escaneie aqui para ver uma tradução em árabe, suaili, quemer, crioulo haitiano e português.

معلومات إضافية: إذا كنت بحاجة إلى مساعدة في استخدام Kinvo، يمكنك الاتصال بخدماتنا عبر الهاتف أو البريد الإلكتروني. نأمل أن تكون هذه المعلومات مفيدة لك. إذا كنت بحاجة إلى مزيد من المعلومات، يرجى الاتصال بخدماتنا عبر الهاتف أو البريد الإلكتروني.

\* KIPEPERUSHI HIKI KIMEUNDWA NA MWANAFUNZI WA PCTA GRAPHICS!